JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA AFYA

BARAZA LA FAMASI

# UTARATIBU WA KUHUISHA VIBALI VYA FAMASI KWA MFUMO WA KILEKTRONIKI

**MWAKA 2024/25**

## A. UTANGULIZI

**1.0 DHUMUNI**: Kutekeleza takwa la Kifungu Na. 36 cha Sheria ya Famasi, Sura 311 (*The Pharmacy Act, Cap* 311).

**2.0 WAHUSIKA**:

- Wafamasia wasimamizi wa famasi husika (Uhuishaji wa Famasi); na
- Fundi Dawa Sanifu (Uhuishaji wa Dukala la Dawa Muhimu la jumla (Accredited Restricted Wholesale – ARW) au Ghala.

**3.0 MFUMO WA UHUISHAJI:** Mfumo wa Kieletroniki utakaomuwezesha Mfamasia Msimamizi au Fundi Dawa Sanifu kuhuisha taarifa na kibali cha jengo husika analosimamia kwa mwaka wa fedha 2024/25. Mfumo wa uhuishaji unapatikana kwa kubofya kiunganishi hapa chini; https://www.pc.go.tz/permit-renewal-apps/

## B. LENGO

Kuboresha ufanisi wa uhuishaji wa vibali na uwasilishaji wa taarifa kutoka kwa wasimamizi. Aidha, mfumo utaokoa muda wa uhuishaji na upatikanaji wa vibali kwa wakati.

### 5.0 UTARATIBU WA KUHUISHA KIBALI CHA KUTOA HUDUMA YA DAWA KWENYE REJESTA

**5.1 FOMU YA KIELEKTRONIKI:**

Mfamasia **ANAYESIMAMIA FAMASI** au Fundi Dawa Sanifu anayesimamia **Duka la Jumla lenye Mipaka** (ARW) au **GHALA LA DAWA** atapaswa kuingia katika akaunti yake aliyofungua awali kwenye kanzidata *(database)* ya Baraza.

**5.2 Mhuishaji:** Anapaswa kubonyeza kitufe cha kuhuisha na kuingiza taarifa zinazohitajika.

**5.3 VIAMBATA: Hakikisha kuwa** nakala zote zinazopaswa kuambatishwa zipo katika Mfumo wa PDF (faili lisilozidi 1.5mb). Nakala za kuambatisha ni kama zifuatazo;

***5.3.1 Mkataba wa makubaliano kati ya mmiliki na mwanataaluma usiopungua muda wa mwaka mmoja (A current signed contract of agreement of Superintendent pharmacist, P/Technician, P/Assistant, P/Dispenser (period of one year)); -***
*Mkataba huu unatakiwa kuwa na:*

*(a) Mandatory terms of referrence yaani majukumu na wajibu wa Mmiliki na Mfamasia Msimamizi kama yalivyoainishwa kupitia [https://www.pc.go.tz/regulations-guidelines/](https://www.pc.go.tz/regulations-guidelines/)*

*(b) Majukumu na wajibu wa kila upande kati ya mmiliki na mwanataaluma mwingine kulingana na wigo wa utendaji wa mwanataaluma husika kama ilivyoainishwa kwenye kanuni ya* ***SUPP GN 267 17 APRIL 2020 -The Pharmacy (Pharmacy Practice and Conduct of Business of a Pharmacy) Regulations, 2020.***

*(c) Muda wa kutoa notisi kwa pande zote mbili usiopungua miezi mitatu (3)*

***5.3.2 Fomu ya uthibitisho endapo mmiliki ni mwanataaluma (A declaration form for pharmacy owners who are pharmaceutical personnel)***
Itajazwa na mwanataaluma ambaye pia ni mmliki wa famasi husika

***5.3.3 Fomu ya kukiri kutekeleza majukumu (A signed commitment form available in the www.pc.go.tz (instead of commitment letter) of registered, enrolled/enlisted or dispenser pharmaaceutical personnel;***

***5.3.4 Mkataba wa mahusiano endapo jengo linamilikiwa na mtu zaidi ya mmoja (Memorandum of Understanding/association (pages that show Directors, identification cards recognized by government for personal identification and their signatures);***

***5.3.5 Nakala ya Cheti cha mlipa kodi (Tax Identification Number (TIN) Certificate) kwa jengo husika;***

***5.3.6 Nakala ya cheti cha jina la biashara lililosajiliwa na BRELA ( Business Name Registration Certificate from BRELA)****;*

**5.4 MALIPO YA ADA YA KUHUISHA KIBALI**

**5.4.1** Baada ya kukamilisha ujazaji wa taarifa na viambata muhimu, mfumo utakupatia **NAMBA YA MALIPO** (***Control Number***) ya kulipia kibali ambayo pia itatumwa kwenye namba ya simu uliyoiingiza.

**5.4.2** Utapaswa kulipia ada hiyo kabla ya muda wa kikomo uliowekwa wa kuhuisha kibali.

**5.5 KUKAMILISHA UHAKIKI:**

**5.5.1** Baada ya uwasilishaji wa taarifa za uhuishaji, uhakiki utafanyika na utakapokamilika utapokea ujumbe wa sms wa kukujulisha upatikanaji wa kibali husika.

**5.5.2** Mfamasia/Fundi Dawa Sanifu (baada ya kupokea ujumbe) atawajibika kurudi kwenye akaunti yake kwa ajili ya kudurufu *(printing)* kibali cha duka husika.

C. **MUDA WA KUHUISHA:** Zoezi la kuhuisha taarifa kwa mwaka wa fedha **2024/2025** litaanza rasmi tarehe **10 Juni, 2024** hadi tarehe **15 Julai, 2024. Ikumbukwe kuwa** baada ya tarehe **15 Julai, 2024** utalazimika kulipa gharama halisi pamoja na **faini ya 25%** ya kiwango ulichopaswa kulipia.

D. **NAMBA ZA SIMU KWA MSAADA:**

| Na | Ofisi za Baraza la Famasi | Namba ya simu |
|---|---|---|
| 1. | **Kanda ya kati na magharibi** (Morogoro, Dodoma, Singida, Iringa**,** Tabora, Kigoma, Katavi, Rukwa) | 0736 222 527 |
| 2. | **Kanda ya Mashariki** (Dar es Salaam, Lindi, Mtwara, Pwani) | 0736 222 523 |
| 3. | **Kanda ya kaskazini** (Arusha, Kilimanjaro, Manyara, Tanga) | 0736 222 531 |
| 4. | **Kanda ya nyanda za juu kusini** (Mbeya, Njombe, Ruvuma, Songwe) | 0736 222 537 |
| 5. | **Kanda ya ziwa** (Geita, Kagera, Mara, Mwanza, Shinyanga, Simiyu) | 0736 222 501 |
| 6. | Makao makuu - Dodoma | 0736 222 515 |

**NB: 1. Taarifa zote zitakazokuwa zimewasilishwa na mfamasia msimamizi endapo zitakuwa si halali, mfamasia husika atachukuliwa hatua za kinidhamu na kisheria.**

**2. Uhuishaji wa vibali kwa maduka ya dawa muhimu (DLDM) utaendelea kufanyika kupitia Ofisi ya Mganga Mkuu wa Halmashauri husika na kuhakikiwa kupitia Ofisi za Kanda kabla ya kuidhinishwa kwa kibali kipya cha Duka (Uhuishaji huu pia utakuwa kwa njia ya mfumo).**

*Imetolewa na:*
**Msajili, Baraza la Famasi**
**S.L.P. 1277,**
**Dodoma**
**Namba ya mawasiliano bila malipo 0800110015**